UNHCR
The UN Refugee Agency

# “HAPA NI NYUMBANI KWETU”

## WALIO WACHACHE WASIO NA UTAIFA NA JUHUDI ZAO ZA KUTAFUTA URAIA



*❝ Fikiria ukiambiwa kwamba hustahili kuwa mahali fulani kwa sababu ya lugha unayozungumza, imani yako, mila zako au rangi ya ngozi yako. Hii ndiyo hali halisi inayowakumba watu wengi wasio na uraia wa nchi yoyote. Pia ubaguzi, ambao unaweza kuwa ndio chanzo cha kimsingi cha ukosefu wa uraia kwao, umeenea katika maisha yao ya kila siku – aghalabu ukiwa na athari zinazolemaza kabisa. Ikiwa tunataka kukomesha hali ya kukosa uraia, sharti tuuondoe ubaguzi huu. Lazima tusisitize kuwepo kwa haki sawa za kitaifa kwa wote. ❞*

**Filippo Grandi**
KAMISHNA MKUU WA SHIRIKA LA UMOJA WA
MATAIFA LINALOHUDUMIA WAKIMBIZI



Ubaguzi. Utengwaji. Uteswaji. Haya ndiyo maneno ambayo kwa kawaida hueleza uwepo wa watu walio wachache na wasio raia wa nchi yoyote. Zaidi ya 75% ya watu wasio na uraia wanaofahamika wanatoka katika makundi ya walio wachache.[1] Watu hawa hujumuisha vizalia vya wahamiaji, wengi wakiwa ni wale waliofika au waliohamishwa kutoka mahali pao hadi kwenye nchi fulani kabla ipate uhuru; watu wanaohamahama kutafuta malisho ya mifugo yao wanaohusishwa na nchi mbili au zaidi; na makundi ambayo yanaendelea kubaguliwa licha ya kwamba wameishi kwa muda mrefu sana mahali hapo wanapochukulia kwamba ndipo nyumbani kwao.

Ubaguzi unaoendeshwa kwa misingi ya kabila, mbari, dini au lugha ni chanzo cha kila mara cha watu kukosa uraia ulimwenguni. Wakati mwingine ubaguzi dhidi ya watu walio wachache umejikita katika sheria: angalau nchi 20 zina sheria za kitaifa ambazo zinaweza kukataza au kupokonya uraia kwa njia ya kibaguzi.[2] Visa vya idadi kubwa ya watu kupokonywa utaifa kwa misingi ya kabila au mbari bado vinaendelea kutokea katika miongo ya hivi karibuni. Mara nyingi, ubaguzi hujikita kwenye sera na desturi rasmi au zisizo rasmi

---

(1) Asilimia hii imetokana na takwimu ya watu wasio na utaifa iliyojumuishwa katika Ripoti ya UNHCR kuhusu Mienendo ya Kimataifa ya 2016 ambayo inafahamika kwamba inahusu kundi la wachache kijamii, kidini au kiisimu. Haihusishi makundi ya wachache ambayo ni sehemu ya watu wasio utaifa katika nchi, ila hayaundi wingi wa idadi hiyo ya watu. Pia asilimia hii haijumuishi makundi mengi ya wachache wasio na utaifa ambao UNHCR haina data ya takwimu kamili kuwahusu.

(2) Tazama Kitendo 4 cha Kamishna Mkuu wa Wakimbizi wa Umoja wa Mataifa (UNHCR), *Global Action Plan to End Statelessness,* 4 Novemba 2014, kinachopatikana: http://www.refworld.org/docid/545b47d64.html



ambazo zinaathiri baadhi ya makundi kwa namna tofauti. Hali ya kutokuwa na uraia wa taifa inaweza kuzidisha utengwaji ambao tayari walio wachache wanakabiliwa nao, ikapunguza zaidi upatikanaji wa elimu, huduma za afya, ajira halali, uhuru wa kwenda popote apendapo mtu, nafasi za kufanya maendeleo na haki ya kupiga kura. Hali hii inaleta tofauti kubwa kati ya makundi yaliyoathiriwa, na jamii pana, huku ikizidisha hali yao ya kuhisi kwamba wao ni wageni: ya kamwe kutokuwa watu wa mahali hapo. Hali hii isiposhughulikiwa, utengwaji wa muda mrefu wa wachache wasio na uraia wa nchi unaweza ukajenga chuki, woga na – katika hali zilizokithiri – usababishe uteswaji, uhamishwaji kutoka mahali wanapoishi, kutotengemaa na ukosefu wa usalama.

Mnamo Mei na Juni 2017, UNHCR ilizungumza na zaidi ya watu 120 ambao wako katika kundi la wasio uraia au kundi la wachache ambao zamani hawakuwa na uraia katika nchi tatu: Wakarana wa Madagaska, Waroma na makabila mengine ya wachache katika Jamhuri ya zamani ya Yugoslav ya Masedonia, na Wapemba na Wamakonde kutoka Kenya. Kutokana na ushuhidi wa kibinafsi uliokusanywa wakati wa mashauriano haya, ripoti hii inaeleza hali ambazo zimesababisha wasitambuliwe kama raia wa nchi yoyote. Inaonyesha jinsi kutokuwa na uraia wa taifa kunaweza kupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, huku watoto wakinyimwa uraia kutokana na chimbuko la kitaifa au kikabila la wazazi wao. Inaangazia aibu na mateso ya kila siku ya watu ambao wametengwa kwa sababu ya sifa ambazo zinafungamana na utambulisho wao – historia zao, sura zao, lugha zao, imani zao. Matokeo ya ripoti hii yanasisitiza umuhimu mkubwa wa walio wachache kufurahia haki za utaifa.

MTINDO WA #IBELONG UMEBUNIWA KWA USHIRIKIANO NA UNITED COLOURS OF BENETTON

**Matokeo haya muhimu yaliyotokana na mashauriano ya UNHCR** na makundi ya wasio uraia na makundi ya wachache ambao zamani hawakuwa na uraia yaliyofanyika mwaka 2017 kuhusu vyanzo na athari za kutokuwa na uraia miongoni mwa vikundi vya wachache vilivyozungumziwa. Matokeo haya yanadhihirishwa kwamba mambo hayo mawili yanaweza kuhusiana kwa karibu (k.m., ubaguzi na kutokuwa na nyaraka za utambulisho zinazohitajika huweza kuwa vyanzo na pia athari za kutokuwa na uraia).

## UBAGUZI

"WATU HUTUAMBIA KWAMBA TURUDI MUMBAI. LAKINI HIYO MUMBAI HATUIJUI. TULIZALIWA HAPA."

—**NASSIR HASSAN,** 48,
JAMII YA WAKARANA,
MADAGASKA

Mara nyingi, ubaguzi na utengwaji wa makundi ya walio wachache kikabila, kidini au kiisimu ndiyo mambo makuu katika hali yao ya kutokuwa na uraia. Wakati huo huo, hali yao ya kutokuwa na uraia inaweza kuwasababishia ubaguzi zaidi, katika sheria na utendaji. Kwa mujibu wa wale ambao tuliozungumza nao, mielekeo ya kiubaguzi inadhihirika katika mahusiano yao na wenye mamlaka na hata wananchi wenzao. Pia wanaripoti kwamba ubaguzi unadhalilisha jamii yao, ukiwazuia kuonekana kama binadamu walio sawa na wengine, na wanaostahili haki na viwango vya heshima sawa na wengine. Aidha, ubaguzi huchangia kuwepo kwa umaskini na matatizo katika upatikanaji wa elimu, huduma za afya, na huduma nyingine za serikali.

## UKOSEFU WA NYARAKA

"WAO [WENYE MAMLAKA] HAWAKUNIELEZA CHOCHOTE, WALIOMBA TU NYARAKA AMBAZO SIKUWA NAZO."

—**HAIDAR OSMANI,** 54,
JAMII YA WAALBANIA, JAMHURI YA ZAMANI
YA YUGOSLAV YA MASEDONIA

Ubaguzi dhidi ya walio wachache wasio na uraia walioulizwa ushauri unajidhihirisha wazi kabisa katika jitihada zao za kupata nyaraka zinazohitajika ili kuthibitisha uraia wao au haki yao ya kuupata uraia huo, kama vile kitambulisho cha kitaifa au cheti cha kuzaliwa. Ukosefu wa ushahidi wa nyaraka kama huo unaweza ukamsababishia mtu matatizo yasiyoisha, ambapo wenye mamlaka wanakataa kutambua dai halali la kupewa uraia. Wakati mwingine, makundi ya walio wachache hupata kwamba haiwezekani kutimiza masharti ya kisheria yanayohitajika ili mtu apewe kitambulisho cha kitaifa – kimsingi, kunahitajika ushahidi kwamba mtu alizaliwa katika nchi anayoishi na mzazi mwenye uraia wa nchi hiyo (k.m. cheti cha kuzaliwa). Hata pale ambapo sheria imeweka bayana kwamba sharti watoto wote wanaozaliwa katika eneo fulani wasajiliwe, kutofahamu sheria kama hizo kunaweza kuwafanya baadhi ya watawala kuyanyima usajili makundi ya walio wachache wanaochukuliwa kuwa wageni. Aina zingine za ubaguzi hujumuisha kukataa bila sababu kutoa nyaraka au kuzisasisha; kutendewa kinyama; au unyanyasaji unaoendelezwa na wenye mamlaka wanaotoa nyaraka. Haya yote husababisha wengi kupanga miadi mara nyingi, kulipa ada za juu na kusubiri muda mrefu mno kabla ya kupata majibu kuhusu maombi ya nyaraka waliyofanya. Watu wengi walioulizwa kutoa maoni walikuwa wamejaribu mara nyingi kupata cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha taifa. Bila kuwa na namna yoyote ya kuthibitisha uraia wao au haki ya uraia, mara nyingi wananyimwa mafao kama vile huduma za afya ya umma na usaidizi wa kijamii unaopewa wananchi.

## UMASKINI

"TATIZO KUBWA NI UMASKINI UNAOSABABISHWA NA HALI YANGU YA KUKOSA URAIA WA NCHI. MTU ASIYE URAIA HAWEZI KUMILIKI MALI. NINAHISI KUDUNISHWA NA KUFEDHEHESHWA NA HALI NILIYOMO."

—**SHAAME HAMISI,** 55,
JAMII YA WAPEMBA,
KENYA

Kutokana na hali yao ya kukosa uraia na ukosefu wa nyaraka zinazohitajika, kwa kawaida makundi yaliyoulizwa kutoa maoni hayakukubaliwa kupata ajira halali au endelevu, au kupata aina ya mikopo au leseni ambazo zingewawezesha kuishi maisha mazuri. Hali hii ngumu inaweza kuwaweka katika hatari ya kutumiwa vibaya kutokana na hali ya unyonge waliyomo na kule kutoweza kupinga mipango ya uajiri ya kiunyonyaji. Huu uwekwaji pembeni unaweza kufanya hali kuwa ngumu kwa walio wachache wasio uraia kuepuka mzunguzko wa umaskini uliopo. Wakiwa wamenyimwa uwezo wa kumiliki mali yao wenyewe, baadhi ya walio wachache wasio na uraia wameamua kusajili mali zao wakitumia majina ya watu wengine (kwa kawaida ya wananchi wanaowafahamu) ili waweze kukimu familia zao, wakibaki katika hali ya kukosa usalama na kujawa na wasiwasi.

## HOFU

"WAO [POLISI] WANAJUA TUNACHOFANYA NA TUNAPOENDA. WANAOMBA VITAMBULISHO VYETU, NA TUNAPOSEMA KUWA HATUNA, TUNATIWA MBARONI NA KUPIGWA."

—**AJNUR DEMIR,** 26,
JAMII YA WAROMA, JAMHURI YA ZAMANI
YA YUGOSLAV YA MASEDONIA

Makundi yote tuliyozungumza nayo yalieleza hofu yao kuhusu usalama wao kwa kuwa wao hawana uraia. Baadhi yao wamepitia mateso ya kimwili ya moja kwa moja. Wengine wametoa mifano ya kulengwa kimakusudi na polisi, na wanaposhindwa kutoa nyaraka zinazohitajika basi hilo linasababisha kutiwa kwao mbaroni au kutoa hongo, pamoja na kuwekwa kizuizini na hata kujaribu kuhamishwa kutoka nchini na wenye mamlaka. Kuchukuliwa kama wahalifu kwa hali ambayo hawawezi kuibadilisha kumeacha wengi wakiwa na makovu ya kisaikolojia na hali ya kuweza kuathirika kwa urahisi. Kwa baadhi yao, kutokuwa na uwezo wa hata kupata mahali pa kudumu pa kuishi au kumiliki mali au rasilimali zao wenyewe ambazo ni za kimsingi katika maisha yao kumewaacha katika hali ya mashaka na wasiwasi mkubwa. Wazazi wote walionyesha kukata tamaa kwa kutokuwa na uwezo wa kubadilisha mustakabali wa watoto wao.

# "TUPO HAPA, HAPA NI NYUMBANI KWETU."

**BACHIR IBRAHIM,** MIAKA 71,
MKARANA WA MAHAJANGA,
MADAGASKA

Kuhakikisha kwamba kuna upatikanaji sawa wa haki za kitaifa kwa makundi ya walio wachache ni lengo mojawapo la #IKampeni ya 'Kustahili kuwa' ya Kumaliza Ukosefu wa Uraia kufikia 2024 ya UNHCR. Ili kutimiza hili, UNHCR inahimiza Mataifa yote kuchukua hatua zifuatazo, kulingana na Vitendo 1, 2, 4, 7 na 8 vya Mpango wa Utekelezaji wa Kimataifa wa Kukomesha Ukosefu wa Uraia wa UNHCR:

- Kuwezesha uandikishaji wa uraia au uthibitishaji wa utaifa kwa vikundi vya wachache wasio na uraia wanaoishi katika nchi mradi tu walizaliwa au wameishi hapo kabla ya tarehe fulani, au wana wazazi au babu/bibi ambao wanatimiza vigezo hivi.
- Ruhusu watoto wapate uraia wa nchi ambamo walizaliwa kama vinginevyo wangekosa uraia.
- Futa sheria na desturi ambazo zinawazuia au kuwanyima watu uraia kwa misingi ya kiubaguzi hali ya kuwa na wazungumzaji wachache wa lugha.
- Hakikisha uwepo wa usajili wa kuzaliwa wa kimataifa ili kuzuia ukosefu wa uraia.
- Ondoa vikwazo vinavyohusu utaratibu na utendaji wa kutoa nyaraka za uraia kwa wale walio na haki ya kuupata kisheria.



MTINDO WA #IBELONG UMEBUNIWA KWA USHIRIKIANO NA UNITED COLOURS OF BENETTON



JAMHURI YA ZAMANI YA YUGOSLAV YA MASEDONIA

**Mnamo Mei na Juni 2017, UNHCR ilizungumza na zaidi ya watu 120** ambao wako katika kundi la wasio uraia au kundi la wachache ambao zamani hawakuwa na uraia katika nchi tatu: Wakarana wa Madagaska, Waroma na makabila mengine ya walio wachache katika Jamhuri ya zamani ya Yugoslav ya Masedonia, na Wapemba and Wamakonde kutoka Kenya. Mashauriano hayo yaliiwezesha UNHCR kuelewa vyema vyanzo msingi vya ukosefu wa uraia katika makundi haya, pamoja na athari ya kutokuwa na uraia katika maisha yao.

Huku kukiwa hakuna data ya kuaminika kuhusu idadi kamili ya watu wasio na uraia ulimwenguni, UNHCR inakadiria kwamba sasa hivi kuna mamilioni ya watu wasio na uraia. Wengi wa watu hawa wako katika kundi ambalo ni la walio wachache kikabila, kidini, au kilugha katika nchi ambazo wameishi kwa vizazi vingi. Kwa hiyo wao ni tofauti na walio wengi kwa sababu hawana uraia na kwa kuwa wao ni wachache.[3] Ripoti hii inazingatia hali ya kutokuwa na uraia na hali ya kuwa wachache na jinsi zinavyoingiliana kupitia kwa tajriba za maisha ya watu.

Katika baadhi ya matukio, ukosefu wa uraia wa mtu husababishwa na sheria za taifa wanaloishi kutowaruhusu kabisa kupata uraia kwa misingi ya hali yao ya kuwa wachache. Kwa mfano, Waislamu wa kabila la Rohingya wanaoishi Myanmar, kundi kubwa zaidi la watu wasio uraia duniani, hawajawekwa kwenye orodha ya 'makundi ya makabila ya kitaifa', ambayo, kulingana na Sheria ya Uraia ya 1982, hupata uraia wa moja kwa moja wakati wa kuzaliwa. Hawawezi kupata uraia wa Myanmar kwa sababu ya jinsi sheria ilivyotungwa na inavyotekelezwa kwa namna ya kiubaguzi. Nchini Syria, katika mwaka wa 1962 takriban Wakurdi 300,000 wa Syria walilengwa kama kundi la kikabila katika sensa maalumu iliyoamriwa kutekelezwa kwa agizo na wakapokonywa uraia wao (idadi hii imepunguzwa hadi kufikia 160,000).[4] Katika hali nyingine, ubaguzi huu hauhusishwi moja kwa moja na hali ya kuwa wachache. Kwa mfano, Mahakama ya Kikatiba ya mwaka 2013 ikitoa uamuzi katika Jamhuri ya

(3) Huku kukiwa hakuna maelezo ya walio wachache yanayokubalika kimataifa, kwa jumla inakubaliwa kwamba walio wachache ni kundi la kabila, dini, lugha, lililo na idadi ndogo kuliko makundi mengine, ambalo wanachama wake wana utambulisho mmoja. Angalia, k.m. Ibara ya 27, Agano la Kimataifa juu ya Haki za Kiraia na Kisiasa.

(4) Hatua muhimu zimeshachukuliwa ili kutatua hali ya Wakurdi wa Syria ambao wamenyimwa uraia wao tangu 1962; hasa, mnamo mwaka 2011 Agizo la 49 lilitangazwa rasmi, na matokeo yake yakawa ni maelfu ya watu wasio uraia kutoka kabila la Wakurdi walio wachache kupewa uraia wa Syria tangu wakati huo.




Dominika ilikuwa na athari mchanganyiko kwa watu wenye asili ya Haiti waliozaliwa katika nchi hiyo, ikiwanyima uraia watu wengi wa kundi hili la walio wachache, hata kama uamuzi uliotolewa haukuwalenga moja kwa moja. Ubaguzi katika desturi za kiutawala katika nchi nyingi unaweza kuyaacha makundi ya walio wachache bila nyaraka kama vyeti vya kuzaliwa na vitambulisho vya kitaifa. Nyaraka kama hizo ni muhimu inapobidi wathibitishe haki yao ya uraia, ikiwaacha wakiwa katika hatari ya kukosa uraia au bila uraia pale ambapo ubaguzi huo ni wa kimfumo na umechagiza. Pale ambapo makundi ya walio wachache ni maskini, wana elimu ya chini kidogo, hawawezi kuzungumza lugha ya taifa, wanaishi katika maeneo ya mbali au hawawezi kupata njia za kufikia ushauri au msaada, basi uwezo wao wa kukabili ubaguzi huu, na utengwaji unaotokana nao, hubaki kuwa mdogo sana.



**Hali ya kutokuwa na uraia inayopitiwa na baadhi ya makundi** ni dalili na pia kisababishi cha kutengwa kwao: inatokana na ubaguzi unaojikita katika tofauti, na inaimarisha hali yao ya kutokuwa wanachama kamili katika jamii wanamoishi, na kuyafanya maisha kuwa magumu zaidi na kuimarisha utengwaji wa kiraia na kisiasa. Wakati mwingine ukosefu wa uraia hueleweka kama tatizo la kiufundi linalotokana na udhaifu wa sheria za kitaifa. Hata hivyo, katika hali nyingi, sababu ya msingi ya makundi ya walio wachache kutokuwa na uraia ni tofauti iliyopo.

Mfumo wa kisasa wa haki za kimataifa wa kuwalinda walio wachache ni juhudi za kutambua na kujaribu kurekebisha hali hii. Haki za walio wachache zinapewa umuhimu mkubwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, ambao unasema katika Ibara ya 27, "Katika Mataifa ambamo walio wachache kikabila, kidini au kilugha wanapatikana, watu wanaotoka katika makundi hayo madogo hawapaswi kunyimwa haki, wakiwa pamoja na wanachama wengine wa kundi lao, ya kufurahia utamaduni wao, kushuhudia na kushiriki katika dini yao, au kuitumia lugha yao wenyewe." Mikataba ya Umoja wa Mataifa kuhusu kutokuwa na Uraia pia ni sehemu ya juhudi za jamii ya kimataifa za kushughulikia hali ya kutokuwa na uraia ulimwenguni.

Mwaka huu ndio kutakuwa na maadhimisho ya 25 ya Azimio la Haki za Watu Walio Wachache katika Taifa au Kabila, Dini na Lugha, ambapo Mataifa yaliahidi kuyalinda makundi haya kutokana na hali yoyote ya ubaguzi. Siku hizi kazi ya Umoja wa Mataifa hujumuisha pia Baraza Maalumu la Haki za Walio Wachache chini ya mwavuli wa Baraza la Haki za Binadamu, Katibu Maalumu wa Haki za Walio Wachache, na maazimio ya mara kwa mara kuhusu mada hiyo yanayotolewa na Baraza la Haki za Binadamu na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Mada kuhusu wachache wasio na uraia lilijitokeza katika Baraza la Haki za Walio Wachache kwa mara ya kwanza mwaka 2016.



**Kutokana na mashauri hayo yote,** UNHCR, pamoja na wawakilishi kutoka kila moja ya jamii za walio wachache zilizoathiriwa, walikutana na washika dau kutoka serikalini na asasi za kiraia ili kuangazia matokeo muhimu. Pia wawakilishi wa walio wachache walisaidiwa ili kutetea hali yao moja kwa moja kwa wenye mamlaka ili jamii zao zijumuishwe kwa kupewa uraia; kuleta mabadiliko ili kuzuia watoto kukosa uraia na kubadilisha sheria zenye ubaguzi; na kuboresha sera na desturi za kiutawala ili kuhakikisha uhuru wa kufikia usajili wa kiraia na ule unaohusiana nao wa kutoa vitambulisho.


Kauli za watu wasio na uraia kutoka kwa makundi ya walio wachache waliozungumziwa katika ripoti hii zinatusaidia kuelewa hali ya ushirikiano changamano iliyopo kati ya hali ngumu ya kuwa walio wachache na kuwa bila uraia. Tukiwa na ufahamu huu, hatua madhubuti zinaweza kuchukuliwa kuondoa udhalimu wa hali ya kutokuwa na uraia na kupunguza magumu ambayo watu wasio na uraia wanapitia katika maisha yao ya kila siku.

Tina Erik, miaka 22, Mmakonde kutoka Kaunti ya Kwale, Kenya, akishiriki katika mashauriano ya watu wachache wasio na uraia Juni 2017.


Mahajanga



# Wakarana wa Madagaska



**SOUGRABAY IBRAHIM, AMBAYE ANA UMRI WA MIAKA 84 NA BADO HANA URAIA, HAJAWAHI KWENDA SHULE.**




**Jamii ya Wakarana, walio wachache nchini Madagaska,** wameishi katika eneo la taifa hili la kisiwa kwa zaidi ya karne moja. Wanasema kuwa chimbuko lao lilikuwa katika mikoa ya magharibi ya India kabla haijagawika, hususan katika eneo ambalo sasa linajumuisha jimbo la Gujarat na sehemu ya Pakistani ya kusini mashariki. Wimbi muhimu kabisa la uhamiaji kutoka India hadi Madagaska lilitokea katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa, wakati ambapo biashara iliyohusisha kusafiri baharini kwenye Bahari Hindi ilikuwa na ushindani mkubwa na watu wengi kutoka India wakatuama Madagaska, hasa katika pwani ya magharibi. Hakuna data ya kuaminika kuhusu idadi kamili ya Wakarana wanaoishi Madagaska; huku ikiaminika na wengi kwamba idadi ya watu hawa walio wachache na wenye asili ya India ni 20,000, huenda idadi yao kamili ni ya juu zaidi. Wengi wa watu hawa walizaliwa Madagaska na maisha yao yote wameishi kwenye kisiwa hicho. Wengi wao wanaishi mijini, ikiwa ni pamoja na mji mkuu, Antananarivo, na mji wa Mahajanga kwenye pwani ya kaskazini magharibi. Ukweli kwamba wengi wa Wakarana ni Waislamu umechangia fikra kwamba wao ni wageni.

“Ili ujiunge na chuo kikuu ulipaswa kufanya huduma ya kijeshi. Bila uraia, sikuweza kufanya huduma ya kijeshi. Na kwa hiyo nimepambana maisha yangu yote bila kuwa na elimu inayohitajika.”

Ingawa idadi kamili haipo, kuna uwezekano kwamba idadi kubwa ya Wakarana wa Madagaska hawana uraia. Hii ni kwa sababu kimsingi sheria ya kitaifa ya Madagaska inazingatia kanuni ya *jus sanguinis* (kutoa uraia kwa watoto ambao wanapozaliwa angalau mmoja wa wazazi wao huwa na uraia wa Malagasi), na kwa jumla Wakarana hawakupewa uraia wakati Madagaska ilipopata uhuru kutoka kwa Ufaransa mwaka 1960 kwa sababu hawakuchukuliwa kuwa wao ni wa kabila la Malagasi. Karibu Wakarana wote wasio uraia waliokutana na maafisa wa UNHCR mwaka 2017 waliripoti kwamba walijaribu kupata uraia wa Malagasi bila mafanikio. Baadhi yao waliajiri mawakili ili kuwasaidia katika juhudi hizi na wakaendelea kuomba uraia kwa miongo mingi bila kupokea jibu rasmi lolote. Idadi isiyothibitishwa ya Wakarana wameweza kupata uraia katika nchi nyingine na hivyo kutatua swala hili la kutokuwa na uraia kwa namna hiyo. Kwa mfano, baadhi ya wale waliokutana na maafisa wa UNHCR walikuwa wamepata uraia wa Ufaransa kupitia kwa mradi ambao Ufaransa ilianzisha wa kuwafaidi baadhi ya wakazi wa makoloni ya zamani ya Ufaransa. Hata hivyo, Wakarana wote waliokuwa na uraia wa Ufaransa ambao maafisa wa UNHCR walizungumza nao bado wanabaki kuwa wakazi wa kudumu wa Madagaska wanaochukulia Madagaska kuwa nyumbani kwao.

Kama ilivyo kwa watu wasio na uraia kote ulimwenguni, mara nyingi Wakarana wasio uraia nchini Madagaska hawawezi kupata elimu rasmi na nafasi za kazi, hali inayowaacha na matumaini yanayodidimia ya kuepuka hali ya umaskini uliokithiri. Ismael Ramjanali, raia mwandamizi ambaye alikuwa hana uraia hadi alipopata uraia wa Ufaransa mwaka 2017, alieleza kwamba kwa kizazi chake cha wanaume, “Ili ujiunge na chuo kikuu ulipaswa kufanya huduma ya kijeshi. Bila kuwa na uraia, nisingalifanya huduma ya kijeshi. Na kwa hiyo nimepambana maisha yangu yote bila kuwa na elimu inayohitajika.” Mama yake, Sougrabay Ibrahim, ambaye ana umri wa miaka 84 na bado hana uraia, hakuwahi kuhudhuria shule. Anakumbuka kwamba alishinda bila chakula ili aweze kuwalisha Ismael na ndugu zake. Ingawa siku nyingi aliweza kuwalisha, hangeweza kuwapa matibabu walipokuwa wagonjwa. Watu walipouliza watoto wake walikuwa na tatizo lipi, ilibidi awajibu kwa kusema, “Wao ni wagonjwa na sina pesa za kuwanunulia madawa.”



“Mimi ni Mwislamu, lakini bila uraia sijawahi kusafiri kwenda Mekka.”

Saguir Ramatoula, miaka 56, Mahajanga, Madagaska.



Aziz Asgaraly kutoka Mahajanga, Madagaska, anawasaidia watoto Wamalagasi walio maskini na yatima katika miradi inayofadhiliwa na jamii ya Wakarana. Hadi sasa, Wakarana wengi bado hawawezi kupata uraia wa taifa lolote. Hati zao za utambulisho wanazopewa na Serikali ya Madagaska zinaonyesha utaifa wao kuwa “usiojulikana” maana yake ni kwamba, kwa uhalisia, hawana uraia.

**Wakarana huzungumzia hali yao ya kutengwa.** Kama Nassir Hassan, mwanamke Mkarana mwenye umri wa makamo, anaeleza hivi, “Watu hutuambia kwamba turudi Mumbai. Lakini hiyo Mumbai hatuijui. Tulizaliwa hapa.” Pia kuna hali ya kukatisha tamaa kutokana na mambo ya kuvunjiwa heshima ambayo wanapitia, ikiwa ni pamoja na vikwazo vingi vya kiutawala ambavyo sharti wavipitie ili kusasisha vitambulisho vyao. Familia ambazo zimekuwa zikiishi Madagaska kwa vizazi vingi bado zinahitaji kupata vibali vya makazi. Kanuni zinabadilika mara kwa mara huku mifumo mipya ya utambulisho, kama vile kitambulisho cha biometri, ikianzishwa, na ada za nyaraka za kujitambulisha zinaonekana kupanda kila wakati. Mahamadhoussen Chamimakatomme, mwanamke Mkarana mwenye umri wa miaka 58, anaeleza jinsi alivyoutafuta uraia wa Malagasi kwa zaidi ya miaka 25. Kama sehemu ya juhudi zake za hivi punde, alilipa kiasi kikubwa cha pesa kwa ajili ya kibali cha ‘muda’ cha makazi cha miaka 100, lakini muda mfupi baadaye akaambiwa kwamba hakikuwa halali ila tu ikiwa kitafanywa upya kwa kutumia biometri. “Kadi yangu ya makazi ilitupwa kwenye jaa na mtumishi wa serikali,” alilalamika. Ibrahim

Ickbal, baba wa watoto wawili mwenye umri wa miaka 50 anayefanyia kazi muuza vito wa eneo lake, hivi majuzi alichukua mkopo kutoka kwa mwajiri wake ili amudu kununua kadi mpya ya makazi ya biometri. “Na huu mshahara wangu wa kawaida, itachukua miaka miwili kuulipa mkopo huo” alisema, kisha akaongeza, “Huu umekuwa uwekezaji mkubwa sana wa kifedha, na bado siwezi kupiga kura au kusafiri”.


> “Tupo hapa. Sisi ni majirani zenu. Inaponyesha, inatunyeshea wote. ua linapoangaza linapaswa kutuangazia sisi sote.”

Hali ya kuvunjika moyo inayotokana na vibali vya makazi vya muda, kubadilika kwa mahitaji ya kupata nyaraka, na ada za juu hudhirika kila mara katika mazungumzo na Wakarana. Baadhi ya watu huambia maafisa wa UNHCR kwamba inawezekana kupewa pasipoti halali za Malagasi kwa ada fulani ili usafiri ng’ambo kwa matibabu, lakini kwamba nyaraka hizi huchukuliwa unaporudi. Hata hivyo, Wakarana wengi wasio na uraia hawawezi kumudu nyaraka hizo za usafiri. Saguir Ramatoula, mwanamume mwenye maneno mazuri aliye na umri wa miaka 56, anaangazia tatizo lisilo la kawaida linalowakumba hasa Wakarana wengi, “Mimi ni Mwislamu, lakini bila uraia sijawahi kusafiri kwenda Mekka”. Anaongeza, “Ikiwa sisi si Wamalagasi kwa kuzaliwa basi sisi ni nani? Hapa ni nyumbani kwetu”.


Aziz Asgaraly, mstaafu mwenye umri wa miaka 60 ambaye anahudumu kama Rais wa Chama cha Jumuiya ya Kodhja pale Mahajanga, anaakisi maoni ya wengi kwamba wanastahili kupewa uraia kutokana na mshikamano wao mkubwa na mchango wao kwa jamii wanamoishi. “Sisi tunaendesha mpango wa kugawa chakula kwa watoto na wazee kila wiki siku ya Jumapili, na tumesaidia kuanzisha shule ambayo inatoa elimu ya msingi na ya upili kwa jamii ya eneo hili. Familia yangu imeishi hapa kwa vizazi vitano lakini nimefanikiwa tu kupata uraia wa Ufaransa, si uraia wa nchi yangu. Kwa nini hatustahili kuwa raia wa hapa?” Sasa watoto wa Aziz pia wana uraia wa Ufaransa kupitia kwake. Anaeleza kwamba kama ilivyo kwa Wakarana wengi waliofanikiwa kwenda ng’ambo kusoma, uwezekano wao kurudi ni mdogo. “Hili linahuzunisha. Mchango ambao wangetoa, uwekezaji ambao tungefanya... watoto wangu wanasoma katika vyuo vikuu bora zaidi ulimwenguni, lakini hawataki kurudi. Kwa nini warudi kwenye nchi ambapo hawana haki? Kama wangerudi wangeistawisha nchi, wangewekeza hapa, lakini hawatarudi. Kwa namna hii tunatoweka jinsi muda unavyokwenda.”

**Licha ya changamoto kubwa** zinazowakabili Wakarana wasio na uraia nchini Madagaska, maendeleo ya hivi majuzi yanastahili kushangiliwa. Mnamo tarehe 25 Januari 2017, Serikali ilitangaza sheria mpya inayotoa hakikisho la kuwepo kwa haki sawa kwa raia, bila kujali jinsia yao, ili kuwatunuku watoto wao uraia. Hii ina maana kwamba kwa sasa, mtoto yeyote anayezaliwa na mama au baba Mmalagasi atatambuliwa kama Mmalagasi. UNHCR wana matumaini kwamba huenda serikali ikachukua hatua zaidi ili kutatua hali ya kutokuwa na uraia ya makundi ya walio wachache. Pamoja na Wakarana, kuna idadi isiyojulikana ya watu wenye asili ya Kichina, Komoro, na wengine wenye asili mchanganyiko ambao hawana uraia nchini Madagaska. Ni watu wachache wanaoweza kukanusha maneno ya Bachir Ibrahim, mwanamume mzee wa Wakarana, ambaye kwa namna sahili lakini yenye mvuto anawatetea Wakarana ili wawe na nafasi sawa za kupata utaifa wa Malagasi: “Tupo hapa. Sisi ni majirani zenu. Inaponyesha, inatunyeshea wote. Jua linapoangaza linapaswa kutuangazia sisi sote.”

# Waroma na makabila ya Jamhuri ya zamani ya



# mengine ya walio wachache
# Yugoslav ya Masedonia







**MIVTAR RUSTEMOV, MIAKA 48** NA
**LIRIJE RUSTEMOV, MIAKA 13**
WA SKOPJE, JAMHURI YA ZAMANI
YA YUGOSLAV YA MASEDONIA

## “NINAHISI MIMI PIA NI WA HAPA.”

**Katika makazi yasiyo rasmi** yaliyo na nyumba za muda, kando na mto Vardar, watoto wa Waroma wanacheza na chupa tupu za plastiki. Makazi haya yanajulikana kama 'Pod Kale', inayomaanisha "chini ya ngome" katika Kimasedonia. "Huwa tunakusanya chupa za plastiki na tunalipwa denari 100-200 kwa siku (chini ya Dola nne za Marekani) lakini hatuwezi kuweka akiba kwa ajili ya siku za usoni. Hatupati usaidizi wowote kutoka kwa Taifa", anaeleza Lasho Nasifi, mwanamume Mroma wa miaka 24 asiye na uraia.

"Hapa ndipo kwetu... hatujatoka kwingine."

Chimbuko la Waroma lilikuwa kule kaskazini mwa India, na walihama kutoka hapo kati ya karne za kumi na tatu na kumi na tano hadi Uropa na hata kufika pale ambapo siku hizi panajulikana kama Jamhuri ya zamani ya Yugoslav ya Masedonia. Waroma ndilo kundi kubwa kati ya makabila ya walio wachache katika nchi hiyo ambao hawana uraia au wako katika hatari ya kukosa uraia. Takwimu rasmi zinaonyesha kuwa kuna Waroma 54,000 nchini, ingawa makadirio yasiyo rasmi yanaonyesha kuwa wapo kati ya 110,000 na 260,000. Waroma wana utambulisho wa kikabila wa kipekee na wanazungumza lugha ya Kiromani pamoja na Kimasedonia, jambo ambalo linawatofautisha na walio wengi wanaozungumza Kimasedonia pekee.

Kutokuwa na uraia kwa Waroma na makabila mengine ya walio wachache kunafungamana, kwa kiasi, na kuvunjika kwa Jamhuri ya Shirikisho la Kisoshalisti ya Yugoslavia mwanzoni mwa mwongo wa 1990. Sheria ya Uraia ya Jamhuri ya zamani ya Yugoslav ya Masedonia, iliyoidhinishwa mnamo Novemba 1992, ilielekeza kwamba raia wa jamhuri iliyotangulia watakuwa raia wa taifa jipya



Watoto Waroma wanacheza katika makazi ya Pod Kale, Skopje, Jamhuri ya Zamani ya Yugoslav ya Masedonia.

lililoundwa moja kwa moja. Wale ambao walikuwa wanaishi kihalali katika eneo la Jamhuri ya zamani ya Yugoslav ya Masedonia wakati wa kuvunjika kwa ushirika wangeweza kupata uraia kwa kutuma maombi ya kuandikisha uraia wao kabla kipindi cha mwaka mmoja kuisha. Wengi walikosa nafasi hii nzuri, kwingi kwa sababu ya kukosa ufahamu, mara nyingi wakiwa hawatambui kwamba wao si raia wa Taifa ambamo wanaendelea kuishi. Kama anavyosimulia Haidar Osmani, Mwalbania wa miaka 54 aliyezaliwa Skopje katika mwaka wa 1963, "Wakati wao [wenye mamlaka] walikuwa wakitoa uraia wa Masedonia, wale ambao hawakujua kuhusu hilo, hawakutuma maombi yao." Matokeo yake ni kwamba wengi wao walikuwa wageni katika nchi walimozaliwa na kuishi karibu maisha yao yote.

Mbali na athari za kuvunjika kwa Yugoslavia ya zamani, ukosefu wa vyeti vya kuzaliwa na aina nyingine za nyaraka za kujitambulisha huathiri sana jamii ya Waroma na upataji wao wa uraia, si tu katika Jamhuri ya zamani ya Yugoslav ya Masedonia lakini pia kote kusini mashariki mwa Uropa. Wakiwa wamenaswa katika mzunguko ambapo ukosefu wa nyaraka kwa wazazi unazuia usajili wa watoto wao, hawana namna ya kuthibitisha haki yao ya kupata uraia. Mara nyingi matokeo yake huwa ni mchanganyiko wa umaskini na kutokuwa na elimu pamoja na ufahamu mdogo wa taratibu na mahitaji ya kupata nyaraka na ubaguzi unaoendelea. Kama anavyoeleza Sherafedin Sejfula, mwanamume Mroma wa miaka 54: "Ubaguzi dhidi ya Waroma umeenea. Upo kila mahali, katika vituo vya polisi, hospitalini, shuleni. Kila mtu ana umuhimu kukuliko. Wao [wasimamizi wa umma] wana mtazamo wa kiburi tangu mwanzo. Daima wanakuambia uondoke. Lakini hii ni nchi yangu, babu/bibi walizaliwa hapa, hatujatoka kwingineko."





**Ukosefu wa nyaraka** hauathiri si tu uwezo wa Waroma wa kuthibitisha au kupata uraia wa Jamhuri ya zamani ya Yugoslav ya Masedonia ila pia unazuia upataji wao wa elimu, huduma za afya, ajira, usaidizi wa kijamii na haki zingine za msingi wanazopewa wananchi. Kizuizi kikubwa katika kupata kitambulisho cha taifa, ambacho ni muhimu katika kufikia huduma za Taifa, ni hitaji la makazi halali ya kudumu. Waroma wengi wanaishi katika makazi yasiyo rasmi au makazi yasiyoidhinishwa, kwa kuwa hawawezi kumudu makazi ya kudumu. Fatmira Mustafa, mama wa watoto wanne, huendesha maisha yake kwa kukusanya takataka kutoka kwenye mapipa. Anaishi kwenye ukingo wa kiunga cha mji cha kaskazini cha Suto Orizari, ambapo kibanda chake kidogo kisicho na maji au sitima kipo karibu na rundo la takataka. Zaidi ya nusu ya jamii ya Waroma wa Skopje wanaishi Suto, kama inavyojulikana katika eneo hilo, manispaa pekee kati ya manispaa kumi za Skopje iliyo na Meya Mroma. Hivi karibuni, Fatmira alielezwa kwamba mwanamume Mwalbania alikuwa amenunua kipande cha ardhi ambapo yeye na familia yake sasa wanaishi kama maskwota. Tangu wakati huo, amekuwa akingojea kwa wasiwasi wakati ambapo mmiliki huyu atabisha mlangoni pake ili amwonyeshe nyaraka ambazo zinampa umiliki wa kipande hicho cha ardhi.

Wale ambao chimbuko lao lilikuwa katika jamhuri nyingine za Yugoslav waliombwa kutoa nyaraka ambazo zinathibitisha kwamba wao si wananchi wa taifa lingine lililotokana na kuvunjika kwa Jamhuri ya Shirikisho la Kisoshalisti ya Yugoslavia. “Wenye mamlaka waliniambia kwamba ilibidi niende Kosovo



Fatmira Mustafa, mwenye umri wa miaka 32, Skopje, Jamhuri ya Zamani ya Yugoslav ya Masedonia.

kupata cheti kitakachoonyesha kwamba mimi si raia wa Kosovo. Lakini ningesafiri kwenda pale vipi bila nyaraka?" anauliza Sutki Sokolovski, mwanamume Mwalbania mwenye umri wa miaka 28. Mama yake, ambaye alimtupa akiwa mtoto, alikuwa anatoka Kosovo lakini yeye alizaliwa katika Jamhuri ya zamani ya Yugoslav ya Masedonia na ameishi hapo maisha yake yote. Waraka pekee aliokuwa nao Sutki ni kitambulisho cha wageni, ambacho huwa hakimpi mtu haki ya kupata bima ya afya na humruhusu tu kuajiriwa kwa muda wa kibali hicho (yaani mwaka mmoja). "Ukiwa na kitambulisho cha wageni, hakuna anayetaka kukuajiri. Tunabaki kuwa maskini", anasema Haidar Osmani. Umaskini, unapounganishwa na kutokuwa na uwezo wa kupata huduma ya afya, una madhara makubwa sana ya afya kwa Waroma wengi ambao hawawezi kulipia bima ya matibabu kutoka kwa mifuko yao wenyewe. Haidar alilazimika kuuza nyumba yake alipohitaji matibabu ya saratani. Akiwa na watu watano katika familia yake, alitakiwa kutoa kama Dola 240 za Marekani kwa mwezi kwa ajili ya bima ya afya. Bila kitambulisho cha taifa, hana haki ya kupata bima ya afya, usaidizi wa kijamii au ajira ya kudumu. "Nimetuma zaidi ya maombi rasmi 20 ya kutafuta nyaraka tangu 1991. Hata nimeitembelea ofisi ya mchunguzi maalumu wa malalamishi ya wananchi. Wao [wenye mamlaka] hawakunifafanulia mambo, waliomba tu nyaraka ambazo sikuwa nazo", alieleza akiwa ameshindwa kabisa.

"Walizaliwa hapa, ninawezaje kukosa kupata vyeti vya kuzaliwa vya watoto wangu?"




Aijnur Demir, umri wa miaka 26 akiwa na familia yake changa katika makazi ya Pod Kale, Skopje, Jamhuri ya Zamani ya Yugoslav ya Masedonia.

Karibu wanachama wote wa jamii hii wanakubaliana na maoni yake kwamba hawapewi maelekezo kamili na wenye mamlaka, kwamba wanatendewa mambo kiholela na kwamba wanaombwa kutoa nyaraka ambazo hawawezi kupata. “Nilienda kwa mthibitishaji rasmi wa umma na nikaomba nyaraka hizi”, Haidar anaendelea, “Hata niliweza kumfanya mthibitishaji rasmi wa umma athibitishe mimi ni nani. Hata nilikuwa na mashahidi. Niliporudi kwa wenye mamlaka kuwaonyesha nyaraka hizo, walisema kwamba sikuzihitaji na wakazirarua.” Bajramsha Esad, mama Mroma mwenye umri wa miaka 42 aliyejaribu kupata cheti cha kuzaliwa cha mtoto wake, anatuambia hivi “wakati afisa mwanamke aliyekuwa kwenye dawati aliponiona aligeuza uso na akaniamuru niondoke. Wanatuudhi, na aghalabu husema ‘Ondoka hapa, mzururaji wewe’.” Hali hii ya kuhisi kuwa wanatengwa kwa sababu ya kabila lao inatawala kwa nguvu katika jamii hii. “Kila wakati ninapoenda mahali ninafukuzwa kwa sababu mimi ni Mroma”, anasema Ferdi Bislimi, mwanamume Mroma mwenye umri wa miaka 23 asiye na nyaraka zozote za kumtambulisha.

**Isipokuwa pale ambapo wameandamana na wakili** au wanasaidiwa na shirika lisilo la kiserikali la mahali hapo, kwa kawaida Waroma hubaguliwa wanapojaribu kupata huduma za umma. Kwa hiyo jamii inalitegemea shirika mwenzi la UNHCR, Chama cha Wanasheria Vijana wa Masedonia, na mashirika yasiyo ya kiserikali ya Roma, kama Ambrela, ili kuweza kupata vyeti vya kuzaliwa na aina zingine za nyaraka na pia kuweza kupata haki zingine, kama vile elimu. Kutokana na majaribio ambayo hayakufanikiwa hapo mbeleni, Waroma wengi wana maoni kwamba hawawezi kuwapeleka watoto wao shuleni. Hata hivyo, Sheria ya Masedonia ya Elimu ya Msingi inaeleza kwamba kila mtoto ana haki ya kupata elimu ya msingi bila ubaguzi wowote. Hii inajumuisha kuwakubali shuleni watoto wasio na uraia na wasio na nyaraka zozote wanaoishi katika nchi hiyo. Katika hali halisi, kwa kawaida watoto wa Waroma huzuiwa kufuzu na kuingia ngazi nyingine ya masomo na sharti vyeti vya kuzaliwa vitolewe ndipo wafanye mitihani ya mwisho. Mivtar Rustemov, baba Mroma aliye na umri wa miaka 48 na mwenye watoto saba, amejaribu kwa miaka mingi kupata vyeti vya kuzaliwa vya watoto wake sita ambao walizaliwa nyumbani. “Siwezi kuelewa jinsi mambo haya yanavyoweza kufanyika. Walizaliwa hapa, ninawezaje kukosa kupata vyeti vya kuzaliwa vya watoto wangu? Ninamtaka [binti yake Lirije] awe na nafasi sawa kama walizo nazo marafiki zake.”

Kizazi cha vijana kinahisi kwamba wanakosa nafasi kwa sababu ya kutoweza kusafiri nje ya nchi au hata kutembea wakiwa huru katika nchi yao kwa sababu ya ukaguzi wa vitambulisho unaowalenga na unaofanywa na polisi. “Wao [polisi] wanajua tunalofanya na tunakoenda. Wanaomba vitambulisho vyetu, na tunaposema kuwa hatuna, wanatutia mbaroni. Wanatupeleka kwenye vituo vya polisi, wanatupiga na kututisha kwamba tutatozwa faini”, anaeleza Ajnur Demir mwenye umri wa miaka 26. Licha ya matamanio ya vijana ya kuepuka fedheha hizi za kila siku, wanakubali kwamba “nchi yetu ni muhimu sana kwetu. Tunahitaji hali nzuri ili tuishi hapa. Kila mahali pengine sisi ni wageni. Hapa tuko nyumbani.”

Sasa, baadhi ya masuala haya yanashughulikiwa. Kikundi Kazi cha ‘Kutatua Suala la Watu Wasiosajiliwa’ kwa msaada wa Wizara ya Kazi na Sera ya Jamii kimerejelea kazi yake hivi majuzi na majadiliano yanaendelea kuhusu uwezekano wa mabadiliko ya sheria ambayo yatawasaidia Waroma kupata taratibu za usajili wa kuzaliwa na wa jina la kibinafsi. Pia Wizara ya Kazi na Sera ya Jamii inalipia gharama ya majaribio ya DNA kwa familia dhaifu sana za Roma ili kuwezesha usajili wa kuzaliwa kwa watoto waliozaliwa nyumbani ambao hawana ushahidi mwingine wa kuthibitisha uhusiano wao na familia zao.


Kaunti ya Kwale



# Wapemba wa Kenya



**SHAAME HAMISI, MIAKA 55,**
KAUNTI YA KWALE, KENYA

## “TUNGEPENDA KUPATA URAIA. HAPA NI KWETU.”



**Maji ya buluu na fuko zinazotoa lulu** ndivyo vivutio vikuu vya wageni kwa pwani ya kusini ya Kenya iliyopambwa ukingoni na minazi. Mashua za kitamaduni za Waarabu zilizotumia tanga na zilizojulikana kama 'Jahazi' kwa Kiswahili, aghalabu huonekana zikikunjua tanga zao za pembetatu mbele ya upeo wa macho – taswira inayotukumbusha historia ya uhamiaji uliofanyika kupitia bahari kati ya Kenya na majirani wake wa pwani. Hata hivyo, maisha si mazuri kwa watu wasio na uraia ambao wameishi katika eneo hili kwa vizazi vingi.

"Tatizo kubwa ni umaskini ambao unaletwa na hali yangu ya kukosa utaifa."

Wapemba, ambao chimbuko lao lilikuwa kisiwa cha Pemba nchini Tanzania, waliwasili kwa mawimbi mawili ya uhamiaji katika pwani ya kusini ya Kenya. Kundi la kwanza liliwasili kati ya 1935 na 1940 wakiwa wanatafuta nafasi bora za maisha. Walitumia kwa manufaa yao uhuru wa kusafiri ambao ulikuwepo baina ya visiwa vya Zanzibar, Pemba na 'Kishoroba cha Maili 10', eneo linalojinyoosha kutoka Vanga karibu na mpaka wa Kenya-Tanzania hadi Kipini huko Lamu, na maili 10 za bahari kuingia bara kutoka kwa ukanda huo wa pwani, sehemu yote ikiwa inatawaliwa na Sultani wa Zanzibar wa wakati huo, Abdullah bin Khalifa. Mnamo mwaka 1963, huku utawala wa wakoloni ukielekea mwisho wake Afrika, Sultani aliachilia udhibiti wake wa Kishoroba cha Maili 10 na eneo hilo likajumuishwa katika Nchi Lindwa ya Kenya. Hivyo basi kikawa sehemu ya Kenya kikamilifu pale ambapo nchi ilipata uhuru mnamo Desemba 1963. Licha ya kuwepo kwa muda mrefu kwa Wapemba kwenye pwani ya Kenya, au ukweli kwamba baada ya muda wengi walikuwa wamepoteza uhusiano wowote waliokuwa nao na kisiwa cha Pemba, hawa wahamiaji wa mwanzo na vizazi vyao hawajawahi kutambuliwa kama wananchi wa Kenya.

Wimbi la pili la Wapemba liliwasili Kenya kati ya 1963 na 1970, baadhi yao wakitafuta nafasi za kiuchumi, lakini wengi wakikimbia vurugu zilizotokana na Mapinduzi ya Zanzibar 1964, ambayo yalipelekea kupinduliwa kwa utawala wa Sultani Jamshid bin Abdullah. Ingawa baadhi ya watu kutoka kikundi hiki walipewa vitambulisho vya Kenya, hivi vilitwaliwa katika enzi gandamizi ya Rais Moi na amri za kuwafukuza nchini Wapemba zilitolewa katika miaka ya miongo ya 1980 na 1990. Licha ya amri hizi, Wapemba wengi walijisitiri katika vichaka nchini Kenya, wakiwa tayari kufanya lolote kubaki katika nchi ambayo walikuwa sasa wanaichukulia kuwa nyumbani kwao. Inakadiriwa kwamba kuna Wapemba 3,500 wanaoishi Kenya leo.

Wakiwa wanaendesha maisha yao kimsingi kupitia kwa uvuvi na kilimo cha mazao ya chakula, kundi la Wapemba 25 wanaume na wanawake wasio na uraia ambalo UNHCR ilishauriana nalo katika kijiji cha Shimoni walikuwa wote waliofika Kenya kabla ya uhuru au watoto wa watu kama hao, waliozaliwa na kukuzwa maisha yao yote katika kaunti za pwani za Kwale na Kilifi. Shaame Hamisi, baba mwenye umri wa miaka 55 na aliye na watoto 13 na ambaye ni Mwenyekiti wa Jamii ya Wapemba, bado hana uraia na hajasajiliwa, licha ya ukweli kwamba mke wake ni Mkenya na anayo haki ya kupitisha uraia wake kwa mume wake kwa mujibu wa sheria. Shaame ni mvuvi na anapitisha siku ndefu zenye jua kali na usiku wa nyota katika Bahari ya Hindi, akijaribu kupata chochote cha kulisha, kuvisha na kuelimisha familia yake kubwa. "Tatizo kubwa ni umaskini ambao unaletwa na hali yangu ya kukosa utaifa" alisema. "Kwa kuwa sina uraia, siwezi kupata leseni ya uvuvi. Bila leseni, siwezi kufanya uvuvi wa bahari ya kina ambapo unaweza kupata samaki wengi. Siwezi kumudu kuwa na mashua yangu mwenyewe, ambayo inagharimu shilingi 300,000 za Kenya (takriban Dola 300 za Marekani), au kuwa na vifaa vya kufaulisha uvuvi. Bila kuwa na kitambulisho cha Kenya, siwezi kuchukua mkopo wa benki ili ninunue

vitu hivyo. Ni lazima nilipe ada ya kukodisha mashua ya jirani yangu na pia nitoe pesa za kuiweka mafuta. Hata kama ningenunua mashua, itabidi niisajili kwa jina la mtu mwingine. Mtu asiye uraia hawezi kumiliki mali. Ninahisi kwamba ninadhalilishwa na kufedheheshwa na hali niliyomo." Si Shaame tu anayehuzunishwa kwa kutengwa. Mekombo Abdallah, mwenye umri wa miaka sitini na sita, ni mwanamke Mpemba asiyezungumza sana, lakini anapoulizwa namna anavyohisi kuhusu hali yake, anasema polepole: "Siwezi hata kula ninapofikiria juu ya hali yangu ya kutokuwa na uraia."

Omar Kombo, mwanamume Mpemba mwenye bashasha aliye na umri wa miaka 48 na watoto sita wadogo, pia anahisi uchungu kuhusu hali ya ukosefu wa usawa anayopitia kutokana na kutokuwa na uraia. Anasema, "Wengi wetu ni wavuvi." "Kitengo cha Usimamizi wa Ufuko hukata shilingi 10 za Kenya kwa kila kilo ya samaki ambayo kila mvuvi aliye kwenye upwa huu anauza. Kituo hiki kinatakiwa kutoa gawio kwa wachangiaji wote kwa ajili ya uharibifu uliozipata mashua wakati wa msimu huo. Kwa kuwa sisi ni Wapemba, hatupati chochote, hata kama mashua zetu zimeharibika. Tunalazimishwa kushiriki katika utaratibu huu, lakini faida yote wanapewa ndugu zetu walio na uraia wa Kenya." Suleiman Ali Makame, mwenye umri wa miaka 40, anayetoka kijiji hicho hicho, anakumbuka wakati ambao alikuwa akivua na Mtanzania huyu kutoka Pemba aliingia kwenye bahari ya upande wa Kenya. "Wote tulitiwa mbaroni na Walinzi wa Pwani ya Kenya na tukaulizwa kutoa vitambulisho vyetu. Nisingeweza, licha ya kwamba nimeishi hapa maisha yangu yote na ninahisi kwamba mimi ni Mkenya. Sijawahi kufika Pemba. Simjui mtu yeyote pale. Nilifungiwa kama mhalifu pamoja na wengine wote."

**Ili kuepuka dosari** ya asili ya kutotambuliwa kama Mkenya, baadhi ya Wapemba wametumia njia za kilaghai ili kukubalika. Bi Aisha Abdallah, mama wa miaka 45 mwenye watoto sita, anakiri kwamba wakati watoto Wapemba wanahitaji kufuzu, baadhi ya wazazi Wapemba wameishia 'kuwanunua' wazazi wa Kenya ambao wanaweza kuwasilisha vitambulisho vya kitaifa ili kuwawezesha watoto hao kufanya mitihani ya kitaifa. Rashid Bakari,* mvulana Mpemba anayejieleza kwa ufasaha, anasema kwamba ana bahati kuwa na uraia. Baba yake aliwasili Mombasa kutoka Pemba mwaka 1938, na alipoulizwa na wenye mamlaka mwaka 1963 kuhusu jadi yake alitaja kabila la Bajuni la mahali hapo, ambapo alikuwa anaishi miongoni mwao. "Lakini mimi si Mbajuni" anasema Bakari, "Mimi ni Mpemba, na hata kama sina tatizo la kukosa uraia, ninataka kurudishiwa utambulisho sahihi wa kabila langu. Ninataka kuwa raia wa Kenya, lakini pia ninataka kuwa mimi jinsi nilivyo." Omar Kombo anakumbwa na mtanziko huo huo na anasema "isipokuwa nibadilishe jina langu hadi kwa lingine linalotumika na kabila la hapa Kenya, sitaweza kusajiliwa kama mwananchi wa Kenya. Lakini ninachagua kutobadilisha jina langu au kabila langu kwa kuwa huo ndio usuli wangu. Mimi ni Mkenya wa asili ya Pemba."

**Katika Katiba ya Kenya** na Sheria ya Uraia na Uhamiaji ya Kenya, watu wasio na uraia ambao wameishi Kenya mfululizo tangu tarehe ya uhuru (12 Desemba 1963), na watoto wao, wanaweza kupata uraia wa Kenya kwa kujisajili. Wageni ambao walifika baada ya uhuru, lakini ambao wameishi nchini Kenya mfululizo kwa miaka saba, pia wana haki ya kupata uraia wa Kenya mradi tu masharti fulani yatimizwe. Kwa hiyo, Wapemba wote na watoto wao ambao maafisa wa UNHCR walishauriana nao wanapaswa kupata uraia wa Kenya.

> "Sijawahi kufika Pemba. Simjui mtu yeyote pale."



Omar Kombo, miaka 48, akiwa na baadhi ya watoto wake, Kaunti ya Kwale, Kenya.



> “Ninataka kuwa raia wa Kenya, lakini pia ninataka kuwa mimi jinsi nilivyo.”

**Hata hivyo,** kutokuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya ushahidi wa kuwasili au tarehe ya kuzaliwa nchini, pamoja na ukosefu wa miundo mbinu ya kutosha ya serikali ili kutekeleza uraia wa kujisajili, umeyaacha baadhi ya makundi ya wasio uraia yanayostahili, kama vile Wapemba, bila ya suluhisho. Kwa wengine, kama mama Maboje Musa, mwanamke wa miaka 90 kutoka Pemba, hii imekuwa na maana kwamba ametengwa kwa karibu karne moja. “Mimi ni mzee kiasi cha kuwa na kilembwe, lakini bado sina uraia,” alisema.

Hata hivyo, kuna ishara kwamba huenda hali hii ikabadilika. Mnamo Desemba 2016, serikali ya Kenya iliwatambua Wamakonde ambao hawakuwa na uraia, kabila lingine linaloishi katika pwani ya Kenya, kama raia, wakiondolewa baadhi ya mahitaji ya kiushahidi na kutoa vitambulisho vya taifa na vyeti vya kuzaliwa japo kuchelewa kwa watu wa jamii hiyo waliostahili. Pia, serikali imeongeza makataa ambayo kwayo watu wasio uraia waliokuwa nchini tangu uhuru, pamoja na vizalia wao, wanaweza kujisajili ili kupata utaifa kuanzia Agosti 2016 hadi Agosti 2019, hili likiashiria utambuzi wa hali inayoendelea ya tatizo hili na kuwa tayari kulitatua. Wanachama wa jamii ya Wapemba wanahamasishana, pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali ya mahali hapo kama Haki Centre lililo na makao yake Mombasa na UNHCR, ili watetee kutambuliwa kwao kama wananchi wa Kenya.




# Wamakonde wa Kenya





**AMINA KASSIM, MIAKA 51,**
KAUNTI YA KWALE, KENYA

## “NILIHISI KAMA MTUMWA. SASA NAHISI KANA KWAMBA NIMEZALIWA UPYA.”



**“Nilihisi kama mtumwa.** Sasa nahisi kana kwamba nimezaliwa upya,” anasema Amina Kassim, mwanamke Mmakonde mwenye umri wa miaka 51, ambaye anaeleza jinsi mtu anavyohisi baada ya kupata uraia wa Kenya na nyaraka baada ya kuishi kama mtu asiye uraia kwa miongo mitano. Furaha na uhakika mpya uliopatikana vinang’ara katika nyuso zao na kupitia kwa sauti za wanachama wengine 30 wa kabila la Wamakonde ambao UNHCR ilishauriana nao huko Ukunda katika kaunti ya pwani ya Kwale. Julieta Simenya, mwenye umri wa miaka 76, ambaye mashavu yake yana ruwaza za chale za kipekee za jadi ya utamaduni wa Wamakonde, wakati mmoja alijificha kwa siku kadhaa na mtoto wake msituni wakati Wamakonde walikuwa wanatiwa mbaroni kwa sababu hawakuwa na vitambulisho vya kitaifa. “Sasa hivi tuna furaha sana” alisema, “Sasa hatuna woga. Sasa machifu wa vijiji kutoka makabila mengine wanatutambua, wanatuamkua, na pia wanatualika kwa mikutano!”

“Ni jambo kubwa sana kwangu kupiga kura kama Mkenya kwa mara ya kwanza baada ya miaka 55.”

Wamakonde wa Kenya ni kabila linalokadiriwa kuwa na watu 4,000 ambao wanaeleza kuwa chimbuko lao lilikuwa Msumbiji kaskazini. Mashauriano na wanachama wa jamii ya Wamakonde, ambao walitambuliwa kama wananchi wa Kenya mnamo Oktoba 2016 baada ya kuishi humu nchini kwa muda mrefu katika hali ya kutokuwa raia, walichunguza kama walikuwa wamepitia mabadiliko yoyote chanya tangu watambuliwe.

Wengi wa watu katika jamii hii ni vibarua ambao waliajiriwa na Mwingereza wakati wa kipindi cha ukoloni ili wafanye kazi katika mashamba ya mkonge na mashamba makubwa ya miwa kote katika kaunti za pwani ya Kenya za Kwale na Kilifi na katika vilima vya Taita Taveta. Wamakonde wengine walio nchini Kenya ni vizali wa wapiganaji wa uhuru waliokimbia kwao na wakimbizi kutoka vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Msumbiji. Licha ya kuwa wengi wameishi Kenya tangu ipate uhuru mnamo Desemba 1963, hawakutambuliwa kama raia au kujumuishwa katika hifadhidata ya usajili wa watu. Ripoti ya sensa ya kitaifa ya 2009 iliwaeleza tu kama ‘wengine’.

Tina Eric, mwanamke mwerevu Mmakonde mwenye umri wa miaka 22, anasimulia kumbukumbu ya kuhuzunisha: “Mmoja wa walimu wangu shuleni alinichagua darasani na akalieleza darasa kuwa mimi ni Mmakonde. ‘Hao ndio wanaokula nyoka’ alisema. Baada ya hapo nilidhihakiwa. Hata wale ambao nilifikiri kwamba walikuwa marafiki zangu hawakunikubali kikamilifu.” Valerian Korneryu, mwenye umri wa miaka 59, anakumbuka siku za kusumbuliwa kila wakati na wenye mamlaka: “Wakati wa utawala wa Moi, nilipewa vitisho na polisi huku wakinielekezea mtutu wa bunduki. Walinishika nikiwa Ukunda na wakanifanya nivue viatu vyangu. ‘Wewe si Mkenya anayestahili kuvaa viatu vya Kenya’ walisema.” Thomas Nguli, Mwenyekiti wa Jamii ya Wamakonde anayeheshimika na aliye na umri wa miaka 60, anathibitisha jinsi hii mielekeo ya kiubaguzi, iliyopo hata katika ngazi za juu sana serikalini, iliishusha hadhi na kuitenga jamii, ikiwazuia kuonekana kama binadamu wenzao wanaostahili kuheshimiwa: “Kiongozi mmoja wa kisiasa aliulizwa jinsi alivyowaona Wamakonde na bila aibu akaeleza umati kuwa aliwaona kama wala watu – watu ambao walikula watu wengine! Baada ya hayo, tulikuwa na matumaini yapi?”

Kwa kweli, kwa muda mrefu Wamakonde hawakuwa na matumaini yoyote. Wasanii wenye talanta, vinyago tatanishi vya mpingo vya Wamakonde kwa muda mrefu vimechukuliwa kama vitu vya thamani vinavyotumiwa kama kumbukumbu na watalii tajiri. Lakini hadi hivi majuzi, kutokuwa na uraia kwao kulimaanisha kwamba mara nyingi



Thomas Nguli, miaka 60, Kaunti ya Kwale, Kenya.

walidanganywa katika kupata mapato sahihi ya kazi zao. “Sisi ndio tulikuwa wachongaji wa kwanza kuuza bidhaa zetu kwenye ufuko” alisema Thomas, “lakini wangekuja na kututia mbaroni, wakisema kwamba hatukuwa na leseni ya kufikia eneo hilo. Ulikuwa ufuko wa umma! Bado, tuliwalipa watu wa kati ambao wangetupa vibali, lakini wangekimbia na kuwaambia polisi ambao wangekuja na kutunyang’anya mapato yetu madogo.” John Hamisi, mwenye umri wa miaka 48, alilipia kitambulisho ghushi cha kitaifa ili apate kazi katika kambi ya safari, lakini bado alilipwa chini ya nusu ya shilingi 18,000 za Kenya (Dola 170 za Marekani) mshahara wa kila mwezi kwa sababu alikuwa Mmakonde. Wakati udanganyifu huu ulipogunduliwa, alifutwa kazi mara moja. “Nilifikiria nijiue, kwa sababu hata kile kidogo ambacho nilikuwa ninapata kama mshahara nisingekipata tena.”

**Bila uraia au nyaraka** za kujitambulisha kama kitambulisho cha kitaifa au vyeti vya kuzaliwa, watoto wa Wamakonde walizuiwa kufuzu kutoka shuleni au kufikiriwa wakati wa kutoa misaada ya masomo. Tina Eric anaeleza jinsi wazazi wake waliokuwa wamevunjika moyo walimruhusu kakake Tina, mwanafunzi mwerevu, aasiliwe na familia ya Kikenya ili aweze kuhudhuria shule ya sekondari. Watu wazima Wamakonde hawakuruhusiwa kupata huduma za kifedha kama mikopo midogo iliyotolewa kwa makundi ya wanawake ili waanzishe miradi ya kufuga nyuki na biashara ya kushona nguo kwa cherahani au mikahawa ya kuuza chai. Amina Kassim analalamika kwamba “kabla ya kupata kitambulisho changu cha kitaifa, niliishi maisha yaliyonidhoofisha. Nisingaliweza kufanya biashara yoyote ya haja. Niliuza vitu vidogo vidogo, kama mandazi ya Waswahili. Hauhitaji

kibali kuuza hayo." Rafiki yake, Khadija Lucas mwenye umri wa miaka 44, anakubaliana naye, akisema "Sikuwa na mtaji. Nisingaliweza kujiunga na vikundi vya kina mama. Ukiwa na kitambulisho cha kitaifa unaweza kukopa hadi shilingi 100,000 za Kenya (Dola 1,000 za Marekani) ili kuanza biashara." Pia uwezo wa kununua mali, kupata huduma za afya au hati za kusafiri haukuwepo. Wote walihisi uchungu wa kutoweza kununua kitu rahisi na muhimu kama simu ya mkononi.

Ingawa wakati uliopita Wamakonde wa Kenya, nyakati mbalimbali, wamealikwa kupiga kura na serikali za Msumbiji na Kenya katika uchaguzi wao, hawajawahi kupewa hadhi ya raia na serikali hizo. Wamakonde walipopata uraia wa Kenya mnamo Oktoba 2016, hilo liliashiria mwisho wa mapambano ya muda mrefu. Mnamo 2015, baada ya miongo mingi ya kufanya ushawishi, jamii ya Wamakonde iliweza kutoa ombi lao kwa Rais Uhuru Kenyatta ili aangalie upya kesi yao. Akiwajibu, alitoa wito kuanzishwe kikundi kazi cha idara mbalimbali ili kuchunguza hali ya kutokuwa na uraia nchini. Kikundi kazi hiki cha mashirika mbalimbali, ambayo yalijumuisha Kurugenzi ya Uhamiaji na Usajili wa Watu, Ofisi ya Usajili wa Kitaifa, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya Kenya, Sekretarieti ya Mambo ya Wakimbizi, Huduma ya Usajili, na Huduma za Taifa za Upelelezi, pamoja na ushauri kutoka UNHCR, kilianza kukusanya data ya kesi na habari kuhusu Wamakonde na makundi mengine yasiyo uraia nchini Kenya kama vile Wapemba (angalia kurasa – weka namba). Mnamo November 2015, Kikundi kazi hiki kilikamilisha ripoti yenye mapendekezo kuwa makundi yasiyo uraia yasajiliwe na wapewe uraia wa kujiandikisha.



Maria Vaz, miaka 55, Kaunti ya Kwale, Kenya.

**Wakiwa wamekata tamaa kwa sababu ya uchelewaji** katika kutekeleza mapendekezo hayo, mnamo Oktoba 2016, mamia ya Wamakonde, wazee kwa vijana, wakisaidiwa na mashirika ya kiraia kama vile Tume ya Kenya ya Haki za Binadamu, walishiriki katika maandamano ya ajabu kutoka Kwale hadi Nairobi ili kumwomba moja kwa moja Rais wa Kenya awatambue kama raia wa Kenya. Mnamo tarehe 13 Oktoba 2016, akiwa ameguswa na taabu na juhudi za Wamakonde, na akiwa amedhamiria kutatua hali yao, Rais Kenyatta aliomba msamaha akisema "imechukua muda mrefu sana kuwapa haki kama Wakenya wenzetu. Leo ndiyo siku ya mwisho kwenu kuitwa wageni." Alitoa agizo kutekeleza masharti yaliyo katika Sheria ya Uraia na Uhamiaji ya Kenya (2011) ambayo inawapa watu wasio raia lakini ambao wameishi nchini Kenya tangu nchi hii ipate uhuru mwaka 1963 (na vizalia wao), haki ya kusajiliwa kama raia wa Kenya. Pia Rais aliwatambua rasmi Wamakonde kama kabila la 43 la Kenya, akiimarisha madai ya vizazi vijavyo vya Wamakonde kutambuliwa kama raia.

> Pia Rais aliwatambua rasmi Wamakonde kama kabila la 43 la Kenya.

Karibu miezi sita baadaye, zaidi ya Wamakonde 1,500 wamepewa uraia wa Kenya. Wamakonde elfu moja mia mbili wamepewa vitambulisho vya kitaifa na 2,000 wamepewa vyeti vya kuzaliwa. Katika harakati hizi, Serikali ilifutilia mbali mahitaji mengi, kama kuonyesha ushahidi kuwa umeishi Kenya mfululizo tangu mwaka 1963, pamoja na ada ya maombi ya shilingi 2,000 za Kenya (Dola 20 za Marekani).

Kwa muda mfupi tangu agizo hilo la Rais kutolewa, athari chanya za kutambuliwa kama raia zinaonekana na jamii. Vijana wa Wamakonde wameajiriwa kama maafisa wa polisi na jeshi na wametengewa nafasi 200 katika Huduma ya Vijana kwa Taifa ili wafanye miradi mbalimbali chini ya mpango wa maendeleo ya kitaifa ya nchi. Uchangamfu wake John Hamisi unakithiri. Amefurahi sasa kwamba "tuna watu wetu ambao wanahusika katika utoaji wa huduma za Serikali. Baadhi yetu wamejiunga na jeshi la polisi. Baadhi yetu wanafanya kazi ya usalama na Kitengo cha Polisi cha Huduma ya Jumla yaani General Service Unit. Ninahisi vizuri kuweza kusimama na kuzungumza kwa lugha ya mama kama Mkenya mwingine yeyote bila kubaguliwa." Wengine wameandikishwa katika mradi wa 'Inua Jamii' ambao unahitaji utume malipo ya pesa kila mwezi kwa simu ya mkononi, ambayo sasa inanunuliwa kwa urahisi, ili kusaidia maisha ya wale walio maskini, wazee au wasiojiweza. Wamakonde wenye umri mpevu walio Mombasa wameandikishwa katika Mfuko wa Bima ya Hospitali ya Taifa, na hili limesaidia wale wanaosumbuliwa na ugonjwa wa kisukari na shinikizo la damu.

Sasa ndugu yake Tina Erik ametimiza miaka 18 na ana kitambulisho cha kitaifa cha Kenya ambacho kimemwezesha kushinda udhamini wa masomo ili akasome katika chuo cha mafunzo ya matibabu. Anatafuta kazi nzuri ambayo itamsaidia "kujenga taifa". Amina Kassim anangojea kwa hamu kupokea pasipoti ili kutimiza ndoto ya maisha yake ya kusafiri India. Tayari Thomas Nguli ameshanunua shamba na anafuatilia hati miliki yake. Maria Vaz anaungojea uchaguzi mkuu kwa hamu: "inamaanisha mengi kuwa ninapiga kura kama raia wa Kenya kwa mara ya kwanza katika miaka 55" anasema. Kwa wanachama 22 wa Kundi la Wachezaji Wamakonde yaani 'Makonde Dancers troupe', hii ni nafasi ya kusajili kundi lao kama biashara, kuonyesha wengine utamaduni wao kupitia kwa utendaji wao na kupata kipato kitakachowawezesha kuwa na maisha mazuri. "Tumefurahi tu" anasema Twi Hamisi mwenye umri wa miaka 33, mmoja wa wachezaji, "sasa, tuko huru".



Hatibu Bakari, miaka 41,
Mpemba, Kaunti ya Kwale,
Kenya.

"TUNAIPENDA NCHI YETU.
TUNAHITAJI HALI NZURI ILI TUWEZE KUISHI HAPA."
"KWA NINI TUNACHUKULIWA KAMA WAGENI NA HATA TUNAAMBIWA TUOMBE VISA ILI TUISHI NYUMBANI KWETU?"
"MAHALI PENGINE POPOTE SISI NI WAGENI.
HAPA TUPO NYUMBANI."

Haya ndiyo maoni yaliyojitokeza sana katika mashauriano kati ya UNHCR na walio wachache wasio na utaifa katika mwaka wa 2017. Ujumbe wenye nguvu zaidi uliojitokeza katika majadiliano hayo ni kuwa walio wachache wasio na utaifa wanahisi kwamba nchi ambazo wameishi kwa vizazi ni zao kama ilivyo kwa raia wengine wa nchi hizo, na wanataka kutambuliwa kikamilifu na kushiriki katika jamii, hali ambayo inaletwa na uraia.

# "HII NI NCHI YETU."

Katika vikundi vya walio wachache vilivyozungumziwa, hakuna waliokuwa wamechagua kutokuwa na utaifa. Wengi walikuwa wamevunjika moyo kutokana na kuvunjiwa heshima walikokuwa wamepitia wakijaribu kupata nyaraka za utambulisho na uraia kwa ajili yao na kwa ajili ya watoto wao, na baadhi wanazidi kunaswa katika juhudi za kuchosha kiuchumi na kisaikolojia za kutafuta utaifa. Kama alivyosema Ismael Ramjanali kutoka jamii ya Wakarana: "Unapata amani ikiwa tu una uraia. Bila utaifa, kutokuwa na usalama kunachukua nguvu nyingi sana." Utengwaji ambao walio wachache wasio na utaifa wanauvumilia huwaathiri sana, lakini pia ni hasara kwa jamii ambamo wanaishi. Huu ndio mtazamo uliochukuliwa, kwa mfano, na Mahakama Kuu ya Bangladeshi mwaka 2008 wakati ilitoa uamuzi mpya kabisa utakaoongoza maswala hayo wa kutambua wazungumzaji wa kiurdu walio wachache na wasio utaifa kama raia wa Bangladesh. Mahakama ilitoa wazo kwamba: "Kwa kuliacha swala la uraia bila utatuzi kwa kushikilia fikra zisizo sahihi kwa miongo, taifa hili halijafaidika kwa namna yoyote – ila limenyimwa mchango ambao wangefanya katika kulijenga taifa."

**Kanuni ya kutokuwa na ubaguzi** ni sehemu ya sheria ya kimataifa, na hati nyingi za haki za binadamu zina vifungu vinavyozingatia haki ya utaifa na haki ya usawa. Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu linatangaza katika Ibara 15 kwamba "Kila mtu ana haki ya utaifa" na "Hakuna mtu atakayenyimwa au kupokonywa utaifa wake au haki yake ya kubadilisha utaifa". Agano la Kimataifa la Haki za Kiraia na Kisiasa linaweka wazi katika Ibara ya 24 kwamba "Kila mtoto ana haki ya kupata utaifa" na katika Ibara ya 26 kwamba "Watu wote wako sawa mbele ya sheria na wana haki, bila ubaguzi, kwa ulinzi sawa wa sheria. Katika hali hii sheria itakataza ubaguzi wowote na ihakikishie watu wote ulinzi sawa na unaofaa dhidi ya ubaguzi kwa misingi yoyote kama mbari, rangi, jinsia, lugha, dini, siasa au maoni mengine, asili ya kitaifa au kijamii, mai, kuzaliwa au hadhi nyingine."

"Unapata amani ikiwa tu una uraia."

Pia kuna vifungu kuhusu haki ya utaifa na kutobaguliwa katika Mkataba kuhusu Haki za Watoto, Mkataba wa Kuondoa Ubaguzi wa Kimbari, na Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake, kati ya vingine. Ibara ya 9 ya Mkataba wa Kupunguza Hali ya Kutokuwa na Utaifa inaeleza kwamba "Taifa linalofanya mkataba halistahili kunyima au kunyang'anya mtu yeyote au kikundi cha watu utaifa wao kwa misingi ya kimbari, kikabila, kidini au kisiasa." Azimio la Haki za Watu Wanaohusika na Taifa, Kabila, Dini, na Walio Wachache Kidini lililokubaliwa miaka 25 iliyopita liliyafunga Mataifa ili yachukue hatua kuhakikisha kwamba watu wanaotoka katika vikundi vya walio wachache wanaweza kutekeleza kikamilifu haki zao zote za kibinadamu na uhuru wa kimsingi bila ubaguzi wowote na kwa usawa kamili kwa mujibu wa sheria. Hivi majuzi, Ajenda ya Maendeleo Endelevu iliyokubaliwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa mwaka 2015 inaakisi uamuzi wa jamii ya kimataifa wa "kutoacha mtu yeyote nyuma", na inayafunga Mataifa kuhakikisha "utambulisho wa kisheria kwa wote, ikiwa ni pamoja na usajili wa kuzaliwa, kufikia 2030" (Target 16.9).

Karibu katika hali zote za kutokuwa na utaifa, suluhisho linalofaa ni kwa watu hao kupewa uraia wa nchi ambayo wana uhusiano mkubwa nayo. Ni muhimu mambo haya yafanikishwe mapema iwezekanavyo katika maisha ya watu binafsi ili waweze kufaidi kutokana na elimu na nafasi zingine ambazo zinaweza kuwapita ikiwa hawana utaifa. Kuhakikisha upatikanaji sawa wa haki za utaifa kwa makundi ya walio wachache ni lengo moja la kimsingi la #IKampeni ya 'Kustahili Kuwa' ili Kumaliza Ukosefu Uraia kufikia 2024 ya UNHCR. Ili kutimiza hili, UNHCR inahimiza

"Sasa tukiwa na uraia, vizazi

Mataifa yote kuchukua hatua zifuatazo kulingana na Vitendo 1, 2, 4, 7 na 8 za Mpango wa Utekelezaji wa Kimataifa wa Kukomesha Ukosefu wa Uraia wa UNHCR:

- Kuwezesha uandikishaji wa uraia au uthibitishaji wa utaifa kwa vikundi vya wachache wasio na utaifa wanaoishi katika nchi mradi tu walizaliwa au wameishi hapo kabla ya tarehe fulani, au wana wazazi au babu/bibi ambao wanatimiza vigezo hivi.
- Ruhusu watoto wapate utaifa wa nchi ambamo walizaliwa kama vinginevyo wangekosa utaifa.
- Futa sheria na desturi ambazo zinawazuia au kuwanyima watu utaifa kwa misingi ya kiubaguzi kama mbari, kabila, dini, au hali ya kuwa na wazungumzaji wachache wa lugha.
- Hakikisha uwepo wa usajili wa kuzaliwa wa kimataifa ili kuzuia ukosefu wa utaifa.
- Ondoa vikwazo vinavyohusu utaratibu na utendaji wa kutoa nyaraka za utaifa kwa wale walio na haki ya kuupata kisheria.

Tangu UNHCR walipozindua #IKampeni ya 'Kustahili Kuwa' ili Kumaliza Ukosefu Uraia kufikia 2024, kuna idadi fulani ya nchi ambazo zimepiga hatua muhimu kulingana na mapendekezo yaliyo hapo juu. Serikali ya Tailandi imetangaza sera ya kitaifa ya kutokuwa na watu wasio na utaifa kufikia 2024 na imethibitisha utaifa wa maelfu ya watu wanaostahili na ambo wanatoka kwa makabila ya vilimani ya walio wachache. Serikali ya Kenya imetatua ukosefu wa utaifa wa muda mrefu wa Wamakonde, ikiwajumuisha kama kabila la 43 nchini Kenya. Serikali ya Malesia imekubali "Mpango makini wa Malesia India" ulio na ufumbuzi wa kitaifa kwa watu wake wenye asli ya India, maelfu ambao utaifa wao wa Malesi umathibitishwa miaka michache iliyopita. Baadhi ya serikali zimeimarisha ulinzi dhidi ya ukosefu wa utaifa kwa watoto, ikiwa ni pamoja na Armenia, Estonia na Tajikistani. Pia jamii ya kimataifa ime imearifu kuhusu uamuzi wake wa kutimiza usajili wa kuzaliwa ulimwengini, na hivyo wasaidie kuzuia ukosefu wa utaifa kupitia kwa kupitishwa kwa Ajenda ya Malengo Endelevu 2030.

**Mengi yanahitaji kufanywa** ili kumaliza ubaguzi na kuhakikisha kuwa makundi yote ya walio wachache yanafurahia haki ya utaifa na manufaa yote yanayotokana nayo. Walio wachache wasio na utaifa wanatafuta tu nafasi sawa na zile ambazo raia wote wanafurahia. Wanapotengwa, si wao tu wanaotaabika, kwa kuwa utengwaji na ubaguzi vina athari hasi za kimaendeleo katika jamii yote. Wakati walio wachache wasio na utaifa wanapotambuliwa kama raia, manufaa huwa wazi. Kwa maneno ya Julietta Simenya, mzee Mmakonde, ambaye zamani hakuwa na utaifa na sasa anatambuliwa kama raia wa Kenya: "Sasa tuna furaha. Sasa hatuna woga. Sasa tukiwa na uraia, vizazi vya baadaye vitakuwa sawa."

vya baadaye vitakuwa sawa."




Ili kulinda utambulisho, majina ya baadhi ya watu waliotajwa katika ripoti hii yamebadilishwa.

Mipaka na majina yaliyoonyeshwa na vyeo vilivyotumiwa kwenye ramani zilizo katika ripoti hii havimaanishi kuwa kuna idhinisho rasmi ua ridhaa ya Umoja wa Mataifa.

Picha ya jalada:
Julieta Simenya, miaka 76, Mmakonde,
Kaunti ya Kwale, Kenya.

Picha zote katika ripoti hii: © UNHCR / Roger Arnold




UNHCR inawashukuru watu walioshiriki katika mashauriano yaliyounda msingi wa ripoti hii. Ukakamavu wa washiriki katika mapambano yao yanayoendelea ili kutambuliwa kuwa raia uliwatia motisha sana washiriki wote wa utafiti. Juhudi za UNHCR zinazoedelea ili kupunguza na kuzuia kuwepo kwa watu wasio na uraia zitafaidika kutokana na taarifa na maarifa muhimu zilizopatikana.

Imechapishwa na Idara
ya UNHCR ya Ulinzi wa Kimataifa

Novemba 2017

Kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi
ya kushiriki katika kampeni ya **#IBelong**,
tafadhali tembelea: www.unhcr.org/ibelong

